# JARIDA LA TLSB

JARIDA LA BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA TANZANIA

TOLEO No. 1 JULAI - DESEMBA 2022


## DKT. MBONI RUZEGEA: MWANAMKE WA KWANZA KUONGOZA BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA TANZANIA (TLSB)



*Dkt. Mboni Ruzegea - Mkurugenzi Mkuu, TLSB*

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) ni Shirika la umma lililopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Shirika hili lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 39 ya mwaka 1963 likijulikana kama Bodi ya Huduma za Maktaba Tanganyika. Mwaka 1975, Sheria hiyo ilirekebishwa ambapo sheria mpya ya Bunge Namba 6 ya mwaka 1975 iliundwa na kupelekea jina la shirika kubadilika kutoka Bodi ya Huduma za Maktaba Tanganyika na kuwa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB).

Lengo kuu la kuundwa kwa TLSB lilikuwa kutoa fursa kwa wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote kutumia Maktaba za umma ili kujipatia elimu, maarifa na taarifa mbalimbali zitakazowasaidia katika kujikwamua kutoka katika umasikini na ujinga na pia kupata burudani na kudumisha utamaduni.

Kufuatia kutungwa kwa sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania mwezi Julai 1963, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliagiza kwamba Mkurugenzi wa Huduma za Maktaba ateuliwe. Mwezi Agosti 1963, Mkurugenzi Edward Maxwell Broome aliajiriwa kutoka Uingereza.

Kwa wakati huo ilikuwa ni lazima kuajiri mtaalamu kutoka nje kwa sababu nchini Tanzania hakukuwa na wazawa walio na taaluma ya Ukutubi. Ilifikiriwa zaidi kuwa mtaalamu huyo atakuwa katika nafasi nzuri ya kuvutia wakutubi zaidi, na pengine kuwepo na uwezekeno wa kupatikana kwa msaada wa kifedha kwa ajili ya maendeleo ya maktaba nchini.

*Inaendelea Uk. 2*

## YALIYOMO


KONGAMANO LA KITAIFA LA HUDUMA ZA MAKTABA, TAMASHA LA VITABU NA USOMAJI LAZINDULIWA ....5

TLSB YAKARABATI MAKTABA ZAKE NCHINI....7

TLSB YASHIRIKI MAONESHO YA KIGODA, NACTVET NA SABASABA ILI KUJITANGAZA....9

BODI YA WAKURUGENZI CHACHU YA MAENDELEO TLSB....11

TLSB YAFANYA MAFUNZO YA RUSHWA NA HIV/AIDS KWA WATUMISHI WAKE.........13

MAKTABA ZA MIKOA ZACHANJA MBUGA KATIKA PROGRAMU ZA UHAMASISHAJI...16



**WAHARIRI**

Dkt. Mboni Ruzegea
Dkt. Rehema Ndumbaro
Dkt. Alfred Nchimbi
Bi. Veronica Bisendo

**MCHAPISHAJI**

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania
S.L.P. 9283, Dar es Salaam,
Tanzania
Tel: 022 2150048/9
Fax: 255 22 2151100
Baruapepe:tslb@africaonline.co.tz
Tovuti: http://www.tlsb.or.tz

**ISSN: 0856 - 2008**

Broome alifuatiwa na Mtanzania marehemu Ezekiel Enock Kaungamno (1971 - 1995), Eliezer Adonia Mwinyimvua (Julai 1996 - 12 Septemba 2005) na Dkt. Alli S. Mcharazo (Mei 2007 – Novemba 2019).
Tarehe 16 April 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan alimteua Dkt. Mboni Amir Ruzegea kwa tangazo lililotolewa na Ofisi ya Rais, Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu mnamo tarehe 19 Aprili, 2022 akiwa ni mwanamke wa kwanza nchini Tanzania kuandika historia kwa kushika wadhifa wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB).

Dkt. Mboni, ni Mkutubi Mbobezi, mwenye Shahada ya Uzamivu ya Sayansi ya Habari na Ukutubi kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kiislam Malasyia (IIUM), kabla ya uteuzi huo, alikua Mhadhiri na Mkurugenzi wa Maktaba Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).
Ni mwaka mmoja tangu Dkt. Mboni Ruzegea ashike usukani wa kuiongoza Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB). Kwa kipindi cha mwaka mmoja tu ameweza kufanya mambo mengi ndani na nje ya TLSB kama ifuatavyo;

## NDANI YA TLSB

Kuanzisha Kongamano la Kitaifa la uboreshaji wa huduma za Maktaba, mafunzo ya ukutubi, tamasha la usomaji na maonyesho ya vitabu. Kongamano hilo kwa mara ya kwanza lilifanyika rasmi tarehe 15 – 17 Novemba, 2021 jijini Dodoma.

Kongamano hilo limeiwezesha TLSB kuwakutanisha washiriki 830 walihudhuria na wengine walipata fursa ya kuwasilisha maoni mbalimbali yatakayosaidia moja kwa moja TLSB kuboresha utoaji wa huduma za maktaba nchini. Wadau




*Pichani: Picha ya pamoja ya viongozi katika ufunguzi wa Kongamano la kwanza la Huduma za Maktaba, Maonesho ya Vitabu na Usomaji lililofanyika jijini Dodoma mwezi Novemba, 2021*

wengine walitazama Kongamano hilo kupitia mitandao ya kijamii kama vile YouTube, Facebook, zoom na tweeter. Taasisi iliandaa kongamano hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kusimamia mchakato wa uundaji wa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Maktaba yaani 'National Policy for Library and Information Services/Sera ya Taifa ya huduma za Maktaba' - Rasimu, ambapo kikao kazi mahsusi kilichoandaa Rasimu hii kilikaa Bagamoyo Mkoani Pwani kikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Dkt. Ruzegea.

Kusimamia mchakato wa kuboresha na kuanzisha utoaji wa huduma za Maktaba nchini kidigitali (e-library), kuwa na Maktaba mtandao ya Taifa (National Digital Library) yenye Katalogi ya Mtandao (Online Public Access Catalogue (OPAC)), Machapisho ya kielektroniki (e - resources), Kanzi data ya machapisho ya kielektoniki (online database) na kuwa na Hazina ya Taifa (National Repository) kwa ajili ya kuhifadhi Bibliographia ya Taifa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Pamoja na kuimarisha uhifadhi wa Machapisho yanayoletwa kisheria (legal deposit) yanajumuisha vitabu kutoka kwa waandishi wa taasisi mbalimbali na watu binafsi, magazeti ya tangu uhuru, indexia za mitihani na hansard za bunge kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa machapisho yenye maudhui ya ndani ya nchi (local content), ambapo hatua hii itarahisisha usomaji kwa watumiaji wote nchini popote walipo na kupata machapisho wanayoyahitaji kwa wakati.

Aidha, Dkt. Mboni ameweza kusimamia zoezi la upatikanaji wa watendaji wa Idara na Vitengo ndani ya taasisi. TLSB kwa muda mrefu, haikuwa na watendaji kabisa katika idara na vitengo kadhaa kama vile kitengo cha Habari na Uhusiano. Wengine ni Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji, Mkuu wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Mkurugenzi idara ya Huduma za Maktaba, Ugavi, Sheria na Tehama. Kwasasa wamepatikana ili kuongeza nguvu ndani ya taasisi.

## NJE YA TLSB

Ziara za usimamizi na ukaguzi katika maktaba za Mikoa ambazo ni; Morogoro, Dodoma, Singida, Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Iringa, Mara Mwanza, Tanga, Lushoto, Manyara, Kigoma, Tabora na Maktaba ya Wilaya ya Chato kwa ajili ya kukabidhi

nyaraka za Ujenzi wa Maktaba hiyo ya Kumbukumbu ya John P. Magufuli. Ziara hizo zimemuwezesha Mkurugenzi Mkuu na Menejimenti kufahamu changamoto zinazozikabili maktaba hizo na kutafuta ufumbuzi..

Ziara Ofisi ya Rais TAMISEMI, ikiwa na lengo la kujenga uhusiano na ushirikiano katika kuendesha huduma za maktaba kwa wananchi. Katika ziara hiyo alikutana na wataalamu wa masuala ya majengo, uhusiano na serikali za mitaa katika jitihada za kuangalia namna kujengewa au kupatiwa maeneo ya kuanzisha huduma za maktaba, vilevile kufahamu majengo yaliyotolewa na serikali za mitaa kwa ajili ya kutumika kutolea huduma za maktaba.Usimamizi na ukamilishaji wa Ukarabati wa majengo ya Maktaba za mikoa ikiwemo: Iringa, Rukwa, Tabora, Kilimanjaro, Kigoma, Kagera na Tabora ambapo kiasi cha Shilingi za Kitanzania 1,059,373,001.95 kimetumika kwa ufadhili wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mradi wa "Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ".
Usimamizi wa zoezi zima la makabidhiano ya jengo la maktaba ya Mbweera kutoka serikali ya kijiji kwenda kwa Taasisi na kupeleka wataalamu (wakutubi) kwa ajili ya kusimamia na kutoa huduma za maktaba katika eneo hilo.

## MAFUNZO



*Pichani: Mkurugenzi Mkuu wa TLSB akizungumza katika Mafunzo ya Uandishi wa Ratiba vyuoni, yaliyofanyika mkoani Morogoro mwaka 2022*

Katika mwaka 2021/22, Dkt. Ruzegea ameidhinisha mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa TLSB hasa katika kujenga uelewa wa pamoja juu mifumo mbalimbali ya serikali ya ulipaji fedha (MUSE), ukusanyaji madeni (GAMS), utunzaji wa samani za serikali (GAMIS), n.k. Mafunzo haya yalifanyika Mkoani Morogoro na kuwawezesha watendaji hasa Wahasibu na Maafisa Ugavi kuweza kuitumia mifumo hiyo kiufasaha.

wa upande mwingine, ametilia mkazo mafunzo ya VVU/UKIMWI na rushwa kwa watumishi, hivyo taasisi imefanya mafunzo hayo sambamba na ushauri wa kupima afya ambapo Watumishi hamsini (50) walishiriki, huku watumishi tisa (9) wanaoishi na VVU/ UKIMWI wamepatiwa msaada wa chakula na virutubishi ili kuboresha afya zao.

Vilevile watumishi 50 wamepatiwa semina ya ufahamu juu ya kupambana na rushwa mahali pa kazi na kuelewa madhara ya vitendo vya rushwa katika kazi.

Semina ya Waastafu; Taasisi imefanya semina hii mwenzi Aprili 2022, Mkoani Morogoro ambapo wastaafu 20 walipatiwa mafunzo hayo, ikiwa ni muda mrefu umepita tangu semina kama hizo kufanyika lakini kwa usimamizi na uongozi wa Dkt. Ruzegea hili nalo limewezekana.

Semina ya Wastaafu ni mafunzo wanayopewa watumishi wa serikali, wizara na idara zake, taasisi na mashirika ya umma mbalimbali kabla ya kustaafu, ili kuwajengea uwezo na ujasiri wa kuyakabili maisha baada ya kustaafu. Maafisa mbalimbali kutoka serikalini wamehusika kuendesha mafunzo haya kwa wastaafu wa wa TLSB kwa mwaka 2021/2022.

## UHUSIANO NA WADAU MBALIMBALI

Kuimarisha uhusiano kati ya Taasisi, na Mashirika, wadau mbalimbali wa maendeleo ambao wamechangia katika kuimarisha utoaji wa huduma za Maktaba ikiwa ni kuiwezesha shughuli ya kongamano, pamoja na kupatikana kwa vitabu, vifaa vya TEHAMA na kupata mafunzo nje ya nchi kwa




*Pichani: Picha ya pamoja kati ya Uongozi wa TLSB na MCT*



*Pichani: Picha ya pamoja kati ya Uongozi wa TLSB na TLA*

watumishi wa Maktaba kwa njia ya mtandao. Miongoni mwa wadau hao ni; Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), 'Book Aid International (BAI)', 'Finnish Library Association (FLA)', Ubalozi wa China, 'Tanzania Education Authority (TEA)', 'Korea International Cooperation Agency (KOICA)', 'Japan International Cooperation Agency (JICA)', 'Taanzania Library Association (TLA)', 'Electronic Information for Libraries – Public Libraries Innovation Programme (EIFL-PLIP)' AFLIA, n.k.

Vilevile, amesimamia uanzishaji wa mahusiano baina ya TLSB na Ubalozi wa Iran nchini. Mnamo tarehe 6 mwezi Mei, 2022, Mkurugenzi Mkuu alikutana na kufanya mazungumzo na Mh. Balozi Hossein Alvandi Bahineh wa Ubalozi wa Iran nchini. Katika Mazungumzo hayo, mambo kadhaa yaliafikiwa kama vile; kuwa na mpango wa kubadilishana (Exchange Programmes) baina ya Wakutubi wa TLSB na Iran na kutoa ufadhili wa masomo kwa wakutubi wa Tanzania kwenda kusoma nchini Iran.

Kusaidia uanzishaji wa Maktaba Mtandao (e-Library) ya TLSB ili nyaraka na vitabu mbalimbali vihifadhiwe kwa teknolojia ya kisasa. Kuanzisha kona ya Iran ya kujisomea itakayokidhi mahitaji ya wasomaji hasa Watanzania. Kubadilishana uzoefu kwa kushiriki maonesho ya vitabu na utamaduni kwa ujumla, nchini Iran na Tanzania na kusaidia kupata mchoro wa jengo la Makao Makuu ya TLSB Dodoma kwa wachora ramani wa Iran (Iran Architects).

Ni dhahiri shahiri yapo mengi na mazuri aliyoyafanya Dkt. Mboni Ruzegea ndani ya mwaka mmoja akiwa madarakani, lakini hayo yote yameweza kufanyika kupitia Serikali ya awamu ya sita, hivyo, shukrani za pekee zimwendee Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa kumteua Dkt. Mboni kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TLSB pia kutenga shilingi bilioni 10.5 kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kuongeza nguvu za kuboresha miundombinu ya jengo la maktaba kuu ya Taifa na maktaba ya Mkoa wa Arusha, vilevile uanzishaji wa maktaba Mtandao, ununuzi wa samani na vitendea kazi na ujenzi wa maktaba ya kumbukumbu ya JPM Chato.

# KONGAMANO LA KITAIFA LA HUDUMA ZA MAKTABA, TAMASHA LA VITABU NA USOMAJI LAZINDULIWA









Kongamano la Kwanza la Huduma za Maktaba Tanzania na Tamasha la Vitabu na Usomaji lilizinduliwa rasmi mnamo mwezi Novemba mwaka 2021 na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mh. Juma Omar Kipanga (MB).

Kongamano hili na Tamasha la Vitabu liliandaliwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) kwa Udhamini Mkubwa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kufanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma kuanzia tarehe 15 hadi 17 Novemba 2021.

Lengo kuu la Kongamano na Tamasha ilikuwa ni kutoa fursa kwa wadau wote wa Huduma za Maktaba nchini kushiriki, kuchangia na kuamua kwa pamoja namna bora ya kuendesha Huduma za Maktaba nchini kwa maslahi mapana ya Taifa.

Pamoja na mambo mengine, Kongamano lilitazama namna matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuandaa, kukusanya, kuchakata, kuhifadhi na kusambaza taarifa inavyoweza kuwa chachu ya mageuzi makubwa ya uboreshaji wa Huduma za Maktaba nchini.

Malengo mahususi ya kongamano na Tamasha yalikuwa ni kutoa elimu kwa wasomaji na wananchi kwa ujumla kuhusu Huduma za Maktaba zitolewazo na Bodi katika Maktaba ya Taifa, Maktaba za Mikoa, Wilaya na Tarafa, na kutambulisha huduma za maktaba zilizoko mashuleni, vyuoni, na kwenye taasisi mbalimbali za mafunzo na utafiti; ili kujenga ufahamu na kuongeza matumizi ya huduma hizi kwa maendeleo endelevu ya nchi na watu binafsi; Kuelimisha na kushirikisha jamii kuhusu mikakati iliyopo ya kuboresha Huduma za Maktaba nchini; Kurahisisha upatikanaji, uhifadhi na usambazaji wa habari na taarifa sahihi kupitia vitabu, majarida, magazeti vilivyomo maktaba kwa wakati ili kukuza tabia ya usomaji; na Kuelimisha jamii kuhusu fursa zipatikanazo ndani ya maktaba.

Kongamano lilikuwa na matukio mbalimbali kama vile; Sherehe za Ufunguzi rasmi wa Kongamano; Uzinduzi wa Vitabu; Uwasilishaji wa Mada

mbalimbali; Washiriki kutembelea Tamasha la Maonyesho ya Vitabu; Majadiliano ya Mada mbalimbali; Kupokea Maoni na Mapendekezo ya Wadau kuhusu Mada zilizotolewa; Kupitisha Maazimio ya Kongamano la Huduma za Maktaba Tanzania; Utoaji wa Tuzo na Zawadi; Kufunga Kongamano; na Washiriki Kutembelea Maktaba ya Bunge la Tanzania, Dodoma.

Maazimio ishirini (20) yaliafikwa katika kongamano hilo kwa ajili ya utekelezaji na mrejesho wa maazimio hayo utaletwa katika kongamano la mwaka huu hapo mwezi Novemba 2022.

Kongamano lilifungwa tarehe 17 Novemba, 2021 na Mgeni rasmi Mhe. Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, akimwakilisha Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Katika Sherehe hizo za kufunga, Mgeni rasmi alikabidhi Tuzo mbalimbali ikiwemo Tuzo ya Heshima kwa familia ya Ezekiel E. Kaungamno aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kwanza Mzawa wa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania. Hii ilikuwa ni kutambua na kuenzi mchango wake katika kuboresha na kuendeleza huduma za Maktaba na Taaluma ya Ukutubi Tanzania.

Halikadhalika Mgeni rasmi alizitunuku vyeti Taasisi zote zilizoshiriki Kongamano hili la kihistoria. Aidha, wawasilishaji wote wa Mada walipewa vyeti kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa na kuwasilisha Mada. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipewa zawadi maalumu kwa kudhamini kongamano.










# TLSB YAKARABATI MAKTABA ZAKE NCHINI

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) imenufaika na fedha za ukarabati kupitia mradi wa **ESPJ** uliopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ndio Wizara mama ya BOHUMATA.

Kupitia mradi huo, Maktaba nane (8) za Mikoa ambazo ni; Maktaba ya Mkoa wa Iringa, Kilimanjaro, Tabora, Kigoma, Morogoro, Rukwa, Kagera na Ruvuma zimenufaika na fedha hizo za ukarabati.

Aidha, Maktaba saba (7), zimekamilika na zinatoa huduma kwa wananchi lakini Maktaba moja (1) ambayo ni Maktaba ya Mkoa wa Kigoma haijakamilika ukarabati wake mpaka sasa. Sababu zilizopelekea Maktaba hiyo kutokamilika kwa wakati ni upungufu wa fedha kutokana na kubadilisha dhana ya ukarabati na kuwa ujenzi sababu ya uchakavu wa jengo hilo.



*Maktaba ya Mkoa - Kilimanjaro*



*Maktaba ya Mkoa - Rukwa*



*Maktaba ya Mkoa - Tabora*



*Maktaba ya Mkoa - Iringa*



*Maktaba ya Mkoa - Morogoro*



*Maktaba ya Mkoa - Kagera (Bukoba)*

# SLADS YAZIDI KUTANUA WIGO WA MAFUNZO

Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) kilianzishwa mwaka 1972 na Wizara ya Elimu wakati huo kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) na kutoa mafunzo ya Astashahada (cheti) ya Ukutubi kupitia chuo cha Ualimu Chang'ombe.

Ilipofika mwaka 1989, Bodi ilianzisha rasmi mafunzo ya Stashahada (Diploma) katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Bagamoyo, kilianza shughuli zake katika majengo ya Chuo cha MANTEP ambacho sasa ni ADEM kabla ya kuhamia Ukuni Bagamoyo katika Majengo yake.

Kwa sasa Chuo kina Kampasi mbili, kampasi ya Bagamoyo na Dar es Salaam na kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE). Kwa miaka thelathini na miwili (32) ya uwepo wa SLADS, kama mwanzilishi wa mafunzo ya fani ya Ukutubi nchini, kimetoa mchango mkubwa katika kudumisha taaluma ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa kuzalisha wataalamu takribani 3,375 kwa ngazi ya Diploma na 4,451 kwa ngazi ya Cheti kuanzia mwaka 1989 – 2020.

Wataalamu hawa wa ukutubi na uhifadhi nyaraka wamekuwa chachu katika kuimarisha usomaji, utafutaji na uchakataji habari, taarifa na maarifa katika ngazi zote za elimu na kwa jamii kwa ujumla na hivyo kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

SLADS inajivunia uzoefu na ubobezi katika fani hii kwani pamoja na uwepo wa vyuo vingi vya umma na binafsi vinavyotoa mafunzo haya kwa sasa, bado wazazi na walezi wanaendelea kukiamini Chuo na kuleta vijana wao kujifunza maarifa haya muhimu.

Kwa mfano, mwaka 2021/2022 SLADS imedahili wanachuo 150 kwa ngazi ya Diploma na 550 kwa ngazi ya Cheti kufanya jumla ya wanachuo 700 sawa na asilimia 70 ya lengo la udahili ikizingatiwa kwamba Chuo hiki kinatoa kozi hii moja tu.

Kwasasa Chuo kimelenga kutanua wigo wake wa mafunzo kwa kutoa kozi za muda mfupi ili kuwawezesha wadau wake kujiendeleza kila kwa kuangalia mahitaji ya jamii kuendana na wakati.

Baadhi ya Kozi hizo ni kama zinavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini;

## RATIBA YA KOZI ZA MUDA MFUPI / TAILORED SHORT COURSES CALENDAR

| S/N | COURSE | VENUE | DURATION | TARGET GROUP |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Online learning/Webinar training | Bagamoyo | 5 days | Librarians, tutors, researchers, and Records officers |
| 2 | Institutional Repository Management | Bagamoyo/Dar es Salaam | 5 days | Librarians, Records managers, Archivists, records clerks, Administrators, Library ICT Personnel |
| 3 | Team Building for information professionals | professionals | 5 days | Directors and Head of deprtments |
| 4 | Managing Libraries and Documentation centres | Dodoma,Bagamoyocenters,Mbeya,Singida | 5 days | Librarians, Periodicals manager, Ward Executive, District /Municipal councilors |
| 5 | Safety and security on Library resources Digital Environment | Tanga | 5 days | Librarians, tutors, researchers, and Records officers |
| 6 | Improving Library services towards digital Environment | Mbeya | 5the days | Librarians |

## TAILORED SHORT COURSES - FOR ONE MONTH CALENDAR

| S/N | COURSE | VENUE | DURATION | TARGET GROUP |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Publishing and printing | Dar es salaam | 1 month | Publishers, Printers, Graduates, |
| 2 | Graphics and Design | Bagamoyo | 1 month | Artists and designers |
| 3 | Basics of Library Skills | Bagamoyo, Dar es Salaam,Dodoma, Morogoro | 1 month | In service personnel in Libraries, Library attendants |

# TLSB YASHIRIKI MAONESHO YA KIGODA, NACTVET NA SABASABA ILI KUJITANGAZA




*Pichani; Mkurugenzi Mkuu wa TLSB Dkt. Mboni Ruzegea akionesha kitabu cha Historia fupi ya Mkoa wa Dar es Salaam kabla ya Uhuru katika maonesho ya Sabasaba 2022*

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) imeshiriki kwenye kongamano la Kimataifa la maonyesho ya Kigoda cha Mwalimu Nyerere yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam tarehe 8 – 10 Juni, 2022.

Mgeni Rasmi katika maonesho hayo alikuwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ni Mkuu wa Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Waliombatana naye ni pamoja na Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Prof. Florens Luoga pamoja na Profesa William Anangisye ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Miongoni mwa shughuli zilizofanywa na TLSB katika maonesho hayo ni pamoja na maonesho ya machapisho mbalimbali yanayomuhusu Hayati Baba wa Taifa Mwl. Nyerere kulingana na dhumuni la maonyesho hayo, machapisho mengine ni; Matokeo ya mitihani ya mwaka 1975, Nukuu za Tanganyika (Tanganyika Notes, sharia za Tanganyika (Tanganyika Law), vitabu vinavyoelezea mila na desturi za makabila mbalimbali ya Tanzania, vitabu vya tafiti ufundi, magazeti mbalimbali ya zamani tangu mwaka 1927 pamoja na fomu za uanachama wa ISBN na ISSN.

Maonyesho hayo yalihudhuriwa na wahadhiri, wanafunzi na wageni kutoka sehemu mbalimbali. Wadau mbalimbali walitembelea meza ya TLSB na kufurahia machapisho yaliyokuwepo.

Aidha, Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi nyaraka (SLADS) kimeshiriki maonesho ya NACTVET ambayo huandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ambapo hapo awali lilijulikana kama Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Maonesho hayo yalifanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 7 Juni 2022 – 13 Juni 2022. Katika maonesho hayo chuo kilionesha na kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa SLADS kama vile; Mafunzo ya Ukutubi kwa ngazi ya Diploma na Cheti na shughuli za Utafiti na Ushauri.

Vilevile, chuo kilitangaza kozi zake mbalimbali za muda mfupi ambazo ziko mbioni kuanza hivi karibuni sambamba na kufanya udahili wa awali kwa wanafunzi.
Kwa upande mwingine, TLSB imeshiriki kikamilifu katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) kupitia Idara na Vitengo vyake vyote. Maonesho hayo yalifanyika katika Viwanja vya Sabasaba Mkoani Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 Juni, 2022 mpaka 13 Julai, 2022.

Miongoni mwa shughuli zilizofanywa na TLSB ni; maonyesho ya vitabu ambavyo ni kiada na ziada, vitabu vya kabla na baada ya uhuru, katiba ya Tanzania, vitabu vinavyoelezea makabila mbalimbali, matokeo ya mitihani, vitabu vya kuchora na kupaka rangi kwa watoto na kutoa huduma za usomaji na michezo kwa watoto Vilevile, Uhamasishaji wa usomaji kwa kutembelea mabanda na sehemu mbalimbali na kusambaza vipeperushi pia kuongea na wadau mbalimbali wanaoweza kushirikiana na TLSB katika shughuli zake.

Uandikishaji wa Wasomaji, Waandishi, Shule na Vyuo wapya, kutoa huduma kwa wenye uhitaji wa namba za ISBN na ISSN na na kufanya utafiti wa vitabu vyenye ISBN na majarida yenye ISSN namba kwenye mabanda ya washiriki wengine.

Aidha, Chuo cha SLADS kilitangaza huduma zake hasa kozi mpya za muda mfupi (Tailored Short Courses), kufanya udahili wa awali kwa wanafunzi, na kufanya utafiti juu ya chuo cha SLADS wakati maonesho yakiendelea.

**Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) yalifunguliwa rasmi na Katibu Mkuu wa eneo huru la biashara Afrika ndugu Wamkele Mene, tarehe 3, Julai, 2022 na Kufungwa na Makamu wa Rais Mh. Philip Mpango tarehe 13 Julai, 2022.**




*Pichani; Matukio mbalimbali katika maonesho ya Kigoda cha Mwalimu, Sabasaba, NACTVET 2022*

# BODI YA WAKURUGENZI CHACHU YA MAENDELEO TLSB



**Prof. Rwekaza Rampho Mukandala**
*Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi*



*Pichani; Wajumbe wa Bodi ya TLSB*

Bodi ya Wakurugenzi ya TLSB inayoongozwa na Prof. Rwekaza Rampho Mukandala imekua chachu ya mabadiliko na maendeleo ndani ya TLSB.

Bodi hiyo kupitia kamati zake tatu ambazo ni; Kamati ya Ajira na Nidhamu, Kamati ya Uchumi, Mipango na Fedha na Kamati ya Maendeleo ya Taaluma zimetekeleza na kusimamia kwa ufanisi mkubwa shughuli mbalimbali ya Taasisi. Kamati ya Ajira na Nidhamu imeshughulikia masuala ya ajira za wafanyakazi, masuala ya nidhamu ya watumishi, na masuala ya ajira na tija ya Bodi.

Kwa upande mwingine, Kamati ya Uchumi, Mipango na Fedha imepokea na kujadili taarifa za mapato na matumizi ya Bodi, kubuni na kushauri kuhusu miradi ya kuongeza vyanzo vya fedha ili kuboresha maendeleo ya Bodi, kusimamia mipango na miradi, kushughulikia mikataba ya ndani na nje ya Bodi, kupokea taarifa za kamati ya Tenda ya Bodi na kushughulikia mipango ya ujenzi TLSB.

Aidha, Kamati ya Maendeleo ya Taaluma, inashughulikia maendeleo yote ya taaluma ya Ukutubi, kufuatilia kwa karibu maendeleo ya Taaluma kuhusu ubora, hadhi na ufanisi wa masomo na chuo, vilevile kupitia mikataba ya ushirikiano wa kitaaluma kwa ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Bodi ya Wakurugenzi ya TLSB inaundwa na wajumbe kumi (10) na Katibu wake ni Mkurugenzi Mkuu wa TLSB.

# UKARABATI NA UJENZI WA MAKTABA ZA TLSB WAANZA

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imenufaika tena na fedha za maendeleo kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia fedha za Miradi ya Maendeleo, kiasi cha shilingi Bilioni kumi na milioni mia tano (TZS 10,500,000,000) zilitengwa kwa ajili ya miradi kadhaa itakayotekelezwa.

Aidha, katika fedha hizo kuna fedha za ukarabati, ujenzi na miradi mingine ya Maktaba, ambapo Jengo la Makao Makuu ya Maktaba Dar es Salaam limetengewa kiasi cha shilingi Bilioni tatu (TZS 3 Bil.) kwa ajili ya Ukarabati.

Kwa upande mwingine, Maktaba mbili zinatarajiwa kujengwa ikiwemo Maktaba ya Kumbukumbu ya JPM Wilayani Chato itakayogharimu kiasi cha shilingi Bilioni tatu na nusu (3.5 Bil.) ambapo makabidhiano ya Nyaraka za ujenzi na eneo yalishafanyika tarehe 14 Julai 2022, pamoja na Maktaba ya Mkoa wa Arusha iliyotengewa kiasi cha shilingi Bilioni tano (TZS 5 Bil.)

Vilevile katika fedha hizi, kuna fedha za miradi ya Maktaba Mtandao kiasi cha shilingi bilioni mbili (2 bil.) na manunuzi ya samani na vifaa vya TEHAMA kiasi cha shilingi Bilioni moja na nusu (TZS 1.5 Bil.).









*Pichani; Makabidhiano ya nyaraka za ujenzi na ukarabati TLSB Dar es Salaam.*

# TLSB YAFANYA MAFUNZO YA RUSHWA NA HIV/AIDS KWA WATUMISHI WAKE





*Pichani: Watumishi wa TLSB wakifuatilia kwa umakini mada mbalimbali zilizowasilishwa katika mafunzo*

Idara ya Utumishi na Utawala ya TLSB imeandaa na kufanya semina kwa watumishi 50 wa Bodi hiyo katika utekelezaji wa mpango mkakati wa Taasisi na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Semina hiyo ikiwa pia ni sehemu ya upimwaji wa utendaji kazi wa Taasisi kupitia mkataba wa makubaliano wa utendaji wa Kazi wa Taasisi (Standard Perfomance Agreement), imefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Bodi ya Huduma za Maktaba Makao Makuu Dar es Salaam.

Lengo la Semina hiyo ilikua ni kuwajengea uelewa watumishi katika masuala ya VVU na Ukimwi lakini pia Watumishi kupata nafasi ya kupima afya zao.

Pia ilitoa fursa kwa watumishi kupewa ushauri nasaha, kujengewa uelewa katika masuala ya Rushwa mahali pa kazi na kujua uhusiano uliopo kati ya rushwa na maadili na kuwapa elimu ya afya watumishi katika kujilinda na magonjwa mbalimbali yanayoweza kutokea kwa kutokuzingatia Lishe bora au ulaji wa chakula sahihi.

Mada mbalimbali zilitolewa kama; Elimu juu ya Rushwa, sababu zinazopelekea kutoa rushwa, athari za rushwa na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa.

Vilevile, Ulaji unaofaa, mlo kamili, Matumizi ya Sukari mwilini na uhitaji wa kiwango cha sukari kinachotakiwa, Uelewa kuhusu ugonjwa wa Ukimwi, kujikinga na huduma zinazotolewa na Serikali katika kupambana na ugojwa huo, na umuhimu wa kupima a afya na kupewa ushauri nasihi.

Baada ya Semina, zoezi zima la upimaji wa afya kwa hiari lilifanyika. Wataalamu wa afya kutoka UMATI waliendesha zoezi la upimaji ambapo watumishi 17 walipima afya na kupewa ushauri nasihi. Kati yao wanaume walikuwa 3 na wanawake walikuwa 14. Idadi ambayo ni sawa na asilimia 34 ya waliopima ukilinganisha na watumishi waliohudhuria semina siku hiyo.

Vile vile, mapendekezo mbalimbali yalitolewa na watumishi baada ya Semina hiyo kama vile; Kuendelea kutoa semina kwa watumishi wengine ambao hawajapata nafasi ya kushiriki. Kuandaa semina inayohusu msongo wa mawazo na jinsi ya kukabiliana nao au kuepuka nao.

Katika Mafunzo watumishi 50 walishiriki kutoka Idara na Vitengo mbalimbali vya TLSB ikijumuisha Chuo cha Ukutubi na Utunzaji Nyaraka (2), Maktaba ya Kibaha (2), Maktaba ya Wasioona (2), Idara ya Huduma za Maktaba (24), Idara ya Fedha (3), Idara ya Utawala (6), Idara ya Mipango (2) Maktaba ya Bagamoyo (1) huku Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani, Ugavi na Manunuzi, Sheria na Miliki vikitoa mtumishi mmoja kila kimoja kushiriki semina hiyo.

Aidha, Mafunzo haya yalitolewa na wawezeshaji kutoka katika Taasisi za Serikali kama vile; TAKUKURU, TACAIDS na UMATI.

# SEMINA YA WASTAAFU YAFANA

Idara ya Utumishi na Utawala ya TLSB imefanya semina kwa watumishi 11, ambapo kati yao watumishi nane (8) wanatarajiwa kustaafu hivi karibuni na watumishi watatu (3) wamestaafu katika utumishi wa umma miezi michache iliyopita.

Semina hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Maktaba ya Mkoa wa Morogoro tarehe 12 - 14 Aprili, 2022, huku Mgeni Rasmi akiwa Dr. Mboni A. Ruzegea, Mkurugenzi Mkuu wa TLSB.

Semina hiyo iliambatana na hafla fupi ya kuaga wastaafu hao ambapo Mgeni Rasmi aliwatunuku vyeti na kuwapa zawadi mbalimbali ikiashiria kutambua na kuthamini mchango wao kwa TLSB.

Aidha, Mgeni Rasmi katika hotuba yake aliwapongeza wastaafu kwa kuwa na utumishi mwema hadi kufikia muda wa kustaafu pia aliwataka kuendelea kufanya kazi mbalimbali binafsi na za kijamii pamoja na mazoezi wawapo nje ya ajira na kutoacha kufanya mawasiliano na Taasisi katika jambo lolote.

Kwa upande wa wastaafu katika hotuba yao ya shukrani, walipendekeza mambo kadhaa ikiwemo; Watumishi wenye taaluma ya ukutubi wapelekwe kwenye vituo/Maktaba ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Taasisi, kufanyike jitihada ya kuhakikisha kunakuwa na Maktaba katika Mikoa yote, ufanyike ukarabati wa majengo, ununuzi wa samani na vitabu kwenye Maktaba zote, kuwekwe vifaa vya kujisomea katika kitengo cha watoto na kutolewe semina ya jinsi ya kuhudumia mteja kwa watumishi TLSB.

Katika semina hiyo mada mbalimbali ziliwasilishwa na wawezeshaji kama vile; uwekezaji na Ujasiriamali, Mafao ya wastaafu kwa mujibu wa Sheria, Bima ya Afya, kuhimili msongo wa mawazo na jinsi ya kutunza afya zao.







*Pichani: Matukio mbalimbali katika Semina ya Wastaafu, Aprili 2022*

# TLSB YAANZISHA UHUSIANO NA IRAN

Bodi ya Huduma, za Maktaba Tanzania (TLSB) imefungua ukarasa mpya wa Uhusiano na Ubalozi wa Iran na kitengo chake cha Utamaduni nchini.

Hayo yamejiri katika kikao baina ya Mkurugenzi Mkuu wa TLSB, Dkt. Mboni Ruzegea na Balozi Hossein Alvandi Bahineh Balozi wa Iran nchini mnamo tarehe 6 mwezi Mei, 2022.

Katika kikao hicho, mambo kadhaa yaliafikiwa kama vile; Kubadilishana mafunzo mbalimbali yaani 'Exchange Programmes' baina ya Wakutubi wa TLSB na Iran na kutoa ufadhili wa masomo kwa wakutubi wa Tanzania kwenda kusoma nchini Iran.

Kusaidia uanzishaji wa Maktaba Mtandao 'e-Library' ya TLSB ili nyaraka na vitabu mbalimbali vihifadhiwe kwa teknolojia ya kisasa. Kuanzisha kona ya Iran ya kujisomea itakayokidhi mahitaji ya wasomaji hasa Watanzania.

Vile vile, kubadilishana uzoefu kwa kushiriki maonesho ya vitabu na utamaduni kwa ujumla, nchini Iran na Tanzania na kusaidia kupata mchoro wa jengo la Makao Makuu ya TLSB Dodoma kwa wachora ramani wa Iran (Iran Architects).

Aidha, Dkt. Ruzegea amemshukuru Mh. Balozi Hossein Alvandi Bahineh wa Iran nchini, pamoja na Kitengo chake cha Utamaduni kupitia Mshauri wake Bwana Morteza Pirani, kwa hatua walioionesha ya kuanzisha uhusiano baina yao na TLSB, hivyo kuahidi kuendeleza uhusiano huo.



*Pichani: Kutoka kushoto, Mshauri wa Kitengo cha Utamaduni cha Iran nchini, Bw. Morteza Pirani, akifuatiwa na Balozi wa Jamhuri ya Kiislam ya Iran Balozi Hossein Alvandi Bahineh, Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa TLSB Dkt. Mboni Ruzegea*





# MAKTABA ZA MIKOA ZACHANJA MBUGA KATIKA PROGRAMU ZA UHAMASISHAJI

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) kupitia idara yake ya Huduma za Maktaba imeendelea kufanya programu mbalimbali (outreach programs) kwa jamii zenye lengo la kuhamasisha usomaji na matumizi ya maktaba hasa kwa wanafunzi.

Vilevile imefanya semina za uandishi wa vitabu na machapisho pamoja na semina za ujasiriamali kwa wadau.

Programu hizo zimefanywa na Vitengo mbalimbali vya Idara ya Huduma za Maktaba na Maktaba za Mikoa, Wilaya na Tarafa ambazo ni miongoni mwa mtandao wa TLSB wenye jumla ya Maktaba 43 nchi nzima.





*Pichani: Matukio mbalimbali katika programu za Uhamasishaji 2022*

# TLSB YAPOKEA WATUMISHI WAPYA WA IDARA NA VITENGO

TLSB imepokea watendaji wapya wa Idara na Vitengo saba (7) katika mwaka 2021/2022 ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Watendaji hao wanaziba nafasi zilizokuwa wazi katika idara na vitengo mbalimbali kufuatia upungufu.

Nafasi hizo ni pamoja na; Mkuu wa Chuo cha SLADS ambapo sasa ni Dkt. Alfred Nchimbi, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji Ndugu Gerald Nzalalila, Mhasibu Mkuu Ndugu Donald Lugelela na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Maktaba Dkt. Rehema Ndumbaro.

Wengine ni pamoja na Bi. Wambura Mkono, Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Ndugu Keneth Sijaona Mkuu wa Kitengo cha Tehama, Ndugu Salim Mbarouk, Afisa Tehama mwandamizi, Ndugu Elirehema Masanja, Afisa Ugavi Mkuu na Bi. Veronica Bisendo, Afisa Habari na Mawasiliano.



Dkt. Alfred Nchimbi
**MKUU WA CHUO - SLADS**



Dr Rehema C. Ndumbaro
**MKURUGENZI WA HUDUMA ZA MAKTABA**



Bw. Donald S. Lugelela
**MHASIBU MKUU**



Bw. Gerald T. Nzalalila
**MKURUGENZI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI**



Bi. Veronica C. Bisendo
**AFISA HABARI NA MAWASILIANO**



Bw. Kenneth S. Sijaona
**MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA**



Bi. Wambura S. Mkono
**MKUU WA KITENGO CHA SHERIA**



Bw. Elirehema Z. Masanja
**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA UGAVI NA MANUNUZI**

# BARAZA LA WAFANYAKAZI TLSB 2022










*Pichani: Matukio mbalimbali katika Baraza la Wafanyakazi TLSB - 2022*

**Tanzania Library Services Board**
Barabara ya Bibi Titi Mohamed,
S. L. P. 9283, DAR ES SALAAM.
Tel: +255-22 2150048/9 +255-22 2151100
Email: info@tlsb.go.tz | Website: www.tlsb.go.tz

tanzanialibraryservicesboard